MWADUI MPYA

Williamson Diamonds Ltd.

A publication of Williamson Diamonds Limited *Vol. 1 Toleo Na. 3* *Februari, 2008*

TAMICO yataja sababu za mahusiano mema kazini WDL



Mojawapo ya vichocheo muhimu vya tija na mahusiano mazuri kazini katika taasisi ya kibiashara ni kuwepo na mashauriano ya mara kwa mara kati ya menejimenti na uongozi wa vyama vya wafanyakazi kuhusu masuala na maamuzi yanayogusa maslahi ya wafanyakazi.

Hii ilitamkwa hivi karibuni na Kaimu Mwenyekiti wa Tawi la Chama cha Wafanyakazi Migodini (TAMICO) mgodini Mwadui, John Kaizilege.

Kaizilege alisema kuwa kuhusishwa mara kwa mara kwa uongozi wa chama cha wafanyakazi katika kubuni na kutekeleza maamuzi yanayohusu maslahi ya wafanyakazi uhamasisha ari na ufanisi wa wafanyakazi kazini, na hupunguza matukio ya migogoro ya kikazi.

Inaendelea Uk. 2

Msimamizi wa zamu kwenye Kinu cha WDL, Aidan Mng'ong'o akiwa kazini kwenye chumba kipya cha usimamizi wa kazi kwenye kinu.(Habari Ukr.3)

WDL yasambaza miche ya miti 33,809

Ukiwa ni mchango wake kwa jitihada za kupanda miti mkoani Shinyanga, mwaka jana Kampuni ya Williamson Diamonds Limited (WDL) ilisambaza miche 33,809 ya miti katika vijiji, shule na taasisi mbalimbali mkoani hapa. Hii ni licha ya miti inayopandwa katika mji wa Mwadui na eneo la machimbo.

Inaendelea Uk. 2

Wakazi wa Kijiji cha Nyasamba, wilayani Kishapu wakipokea miche ya miti iliyotolewa bure na Kampuni ya Williamson Diamonds Ltd. hivi karibuni.

Be Passionate — Penda Kazi kwa Dhati

Pull Together — Tushikamane

Build Trust — Jenga Uaminifu

Show We Care — Tuonyeshe Kuthaminiana

Shape the Future — Kutengeneza Maisha ya Baadaye

Dira ya Williamson Diamonds Ltd. ni kutambulika kama bingwa katika kuchimba udongo wenye almasi wa gredi ya chini

TAMICO yataja sababu za mahusiano mema

Inatoka Uk. 1

Aliipongeza menejimenti ya sasa ya WDL kwa kuweka utaratibu wa kupata ushauri na maoni ya uongozi wa chama cha wafanyakazi katika kufanya maamuzi yanayogusa maslahi ya wafanyakazi na shughuli za uzalishaji mgodini

Miongoni mwa mifano ya ushirikiano kati ya menejimenti ya WDL na uongozi wa tawi la TAMICO ni mkataba uliofikiwa na pande hizi mbili mapema mwaka 2007 ili kukabili tatizo la kukwama kufikiwa malengo ya uzalishaji ya mwaka huo.

Ili kupunguza malengo kutofikiwa, ilikubaliwa kwamba katika mwaka huo kazi za uzalishaji hazitasimama wakati wa sikukuu.

Kaimu Mwenyekiti wa Tawi la TAMICO alisema kuwa uongozi wa sasa wa chama hicho, ambao ulichaguliwa mwaka 2006, mara kwa mara hujadiliana na wafanyakazi kabla na baada ya kushauriana na menejimenti kuhusu masuala yanayogusa maslahi yao.

Alisema kuwa chini ya uongozi wao kumepungua kesi za utovu wa nidhamu zinahusisha wafanyakazi wa WDL.

Alisema kuwa hii imetokana na jitihada za uongozi wa tawi kujadiliana na wafanyakazi kuhusu matatizo yanayojitokeza kwenye sehemu za kazi na haja ya kuzingatia sheria za kazi na kanuni za kampuni.

Hivi sasa tawi la TAMICO mgodini Mwadui lina wanachama 400.

Vifo vyagubika msimu wa sikukuu Mwadui

Msimu wa sikukuu wa mwishoni mwa mwaka ulikuwa ni wa majonzi kwa menejimenti ya WDL na jamii nzima ya mgodi kutokana na vifo vya wafanyakazi wanne wa kampuni vilivyotokea ndani ya kipindi cha miezi miwili.

Hamzuruni Kilao, aliyekuwa fundi mchundo, alifariki kwenye Hospitali ya Mwadui mnamo Novemba 23, mwaka jana, akiwa na umri wa miaka 45.

Mazishi yake yalifanyika Nyamanoro, Mwanza na ameacha mjane na watoto wawili.

Mnamo Desemba 25, mwaka jana, mfanyakazi kwenye kinu, Emmanuel Maganga (55) alifariki kwenye Hospitali ya Mwadui baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Marehemu alizikwa nyumbani kwao Puge, Nzega, mkoani Tabora na ameacha mjane na watoto tisa.

Dominick Mhoja, aliyekuwa fundi mchundo katika karakana, aliaga dunia kwenye Hospitali ya Mwadui, Januari 5, mwaka huu, baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Mazishi yake yalifanyika nyumbani kwao kijijini Msalala, Geita, mkoani Mwanza. Ameacha mjane na watoto wane.

Mnamo Januari 14 mwaka huu, msimamizi wa nyumba za wageni za kampuni, Kiyenze Msabila (45) alifariki kwenye Hospitali ya Mgodi.

Mazishi yake, ambayo pia yalihudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa WDL, Tony Devlin, yalifanyika kijijini kwao Utwigu, mkoani Tabora. Marehemu Msabila ameacha mjane na watoto saba.

Williamson Diamonds Limited.
Mwadui, Shinyanga Region, Tanzania
P. O. Box 9470,
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 28 2763872
Fax: +255 28 2762965
Email:wdl@wdl.co.tz

Wafanyakazi wapya WDL

Juma Deresu Malunga (38) amejiunga na WDL kama Meneja wa Idara ya Usalama, Afya na Mazingira, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Bertus Stoker ambaye ameacha ajira ya kampuni hivi karibuni.

Malunga ana shahada ya kwanza ya sayansi (pamoja na elimu) na shahada ya uzamili katika kemia ya mazingira migodini, akiwa amewahi kushikilia nafasi za juu kwenye fani hiyo kwenye migodi mbalimbali nchini Tanzania na Marekani. Ameoa na anao watoto wawili.

Juma Deresu Malunga

Albert A.Mongi hivi karibu alijiunga na WDL kama Mjiolojia kujaza nafasi ya Javan Enock, aliyejiuzuru mwezi Juni 2007. Mongi anayo shahada ya kwanza ya jiolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam..

Michael Cheche na Iddi S. Amiri wamejiunga na WDL Desemba 2007 kama Wahasibu Wasaidizi.

Cheche anacho cheti cha uhasibu ya CPA, stashahada ya juu ya uhasibu na stashahada ya uzamili ya maendeleo ya ushirika. Ameoa na ana watoto wanne.

Amiri anayo shahada ya biashara (uhasibu) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. .

Albert A. Mongi

WDL yasambaza miche ya miti 33,809

Inatoka Uk. 1

Idara ya Usalama, Afya na Mazingira ya WDL ndiyo inayosimamia kutunza kitalu ambako miche ya miti inaoteshwa. Meneja wa idara hiyo, Juma Malunga, amesema kwamba miche imesambazwa kwenye, ambayo inahusika na uendeshaji wa kitalu cha miche ya miti cha kampuni.

Meneja wa idara hiyo, Juma Malunga, amesema kuwa miche hiyo ilisambazwa kwenye vijiji vitatu wilayani Kishapu (miche 3,882), shule 15 za msingi (miche 15,846), shule tisa za sekondari (miche 12,650) na taasisi nne (miche 2,364).

Malunga ameeleza kwamba WDL inakusudia kupanua kitalu cha miche ili kiweze kuotesha miche 500,000 mwaka 2008. Miche hii baadaye itapandwa kwenye maeneo ya mji na machimbo hapa Mwadui na mingine itasambazwa kwa jamii zilizopo jirani na mgodi.

Meneja huyo wa Idara ya Usalama, Afya nma Mazingira amesema wanatarajia kuanzisha vitalu vya miche ya miti ya mbao, kuni na matunda vijijini na kuendesha mafunzo kwa wanavijiji kuhusu jinsi ya kuitunza.

Idara yake Malunga pia ina mpango wa kuvisaidia vijiji jirani na Mwadui kuanzisha vitalu vyao vya miche vitakavyootesha miti ya matunda, mbao na kuni. Hii pia itajumuisha kutoa mafunzo kuhusu mbinu za kuotesha miche na kutunza miti.

Wakati huo huo, WDL inaandaa siku ya kupanda miti ya katika "Mwadui Mpya" mnamo Jumamosi, Februari 16, mwaka huu. Wito wa siku hiyo ya kupanda miti ni: "Kuwa na tabia ya kupanda miti na tunza mazingira."

Zaidi ya miche 4,000 ya miti ya asili itapandwa mgodini, hususan kwenye eneo jipya la hifadhi, ambalo hapo awali lilikuwa uwanja wa mchezo wa gofu. Jamii nzima na wanafunzi wa shule zote zilizopo Mwadui wanakaribishwa kushiriki katika shughuli zitakazofanyika siku hiyo.

.Aidha, Meneja wa Idara ya Usalama, Afya na Mazingira amewahimiza wakazi wa Mwadui kupanda miti ya matunda na maua kwenye maeneo ya nyumba zao na amesema kuwa miche ya miti ya aina hiyo inapatikana bure kwenye kitalu cha miche cha Mwadui.

Ikitokea tukio la moto wasiliana mara moja na maafisa wafuatao:

Mkuu wa Zimamoto	-	0784 445 936
Meneja, Usalama, Afya na Mazingira	-	0784 771 009
Mratibu, Afya Kazini	-	0754 490 153
Ofisi ya Usalama, Afya na Mazingira	-	2762564
Ofisi ya Securicor	-	2762478
Kinu cha Umeme	-	2762539

Usimamizi wa kutumia mitambo kutaboresha uzalishaji

Ikiwa ni sehemu ya kutekeleza kanuni bora za kazi katika shughuli za uzalishaji, WDL imejenga chumba kitakachorahisishia maopereta na wasimamizi kusimamia na kuongoza kazi katika kinu cha kusafisha mchanga wenye almasi.

Kwa mujibu wa Meneja wa Kinu, John Chandler, chumba hicho kimejengwa kwenye sehemu inayowawezesha wasimamizi kuona kazi zinavyoendelea kwenye maeneo yote ya kinu.

Zaidi ya hiyo, kwa kutumia mtandao wa kamera kuona maeneo muhimu kwenye kinu na mengine yasiyo rahisi kuonekana, chumba hicho kimeboresha uratibu wa shughuli za uzalishaji.

Kupitia televisheni zilizopo kwenye chumba hicho, kilichopo juu ya mtambo wa DMS, mtu anaweza kuona vyema shughuli mbalimbali zinazoendelea kwenye kinu.

Chandler amesema kuwa hapo awali ilibidi msimamizi azunguke huku na huko kwenye kinu ili aweze kufahamu kazi zinavyoendelea.

Sasa msimamizi anakuwa na picha kamili ya jinsi kinu kinavyofanya kazi na anaweza kuhakikisha kwamba timu yote ya wafanyakazi kwenye kinu inafanya kazi kwa ufanisi kama kundi moja. Hii itajenga ushirikiano katika kutatua matatizo na kupunguza kukwama kwa uzalishaji.

Chandler amesema utataribu wa zamani ulisababisha wafanyakazi wa vitengo mbalimbali kutoshirikiana, akiongeza kuwa hali hii mara nyingi ilisababisha kazi za uzalishaji kuzorota.

Meneja wa Mgodi, Danie Smit, amesema kwamba kujengwa kwa chumba cha usimamizi wa shughuli za kinu kutasaidia sana kuboresha usimamizi na kutawaandaa wasimamizi kufanya kazi katika kinu kipya kinachopendekezwa kujengwa.

Hivi sasa na WDL ndiyo kampuni pekee kwenye familia ya makampuni ya De Beers yenye kinu kisichokuwa na mitambo ya kujiendesha yenyewe.

Shule ya Msingi Mwadui 'A' ni moja ya shule nne za msingi wilayani Kishapu zilizotuzwa mipira na Tawi la Mwadui la Benki ya National Microfinance. Meneja Uendeshaji wa Tawi, Barthromew Mahangaiko (wa kwanza kulia) na Afisa Mikopo wa Tawi, Joyce Bangi (wa pili kulia) wakikabidhi mipira kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Peter Leonard, afisa mwanafunzi kwenye Idara ya Kompyuta ya WDL, hivi karibuni alifuzu masomo ya Stashahada ya Juu ya Teknolojia ya Mawasiliano kwenye Chuo cha Uhasibu Arusha.



Mwadui 'A' yang'ara mitihani ya taifa

Katika mafanikio yaliyovunja rekodi, wanafunzi wote 61 waliofanya mtihani wa taifa wa kumaliza darasa la saba kwenye Shule ya Msingi Mwadui 'A', wamefaulu na wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule mbalimbali za sekondari za serikali.

Zaidi ya hiyo, mwaka jana wanawafunzi wote 53 wa shule hiyo walishinda kwa gredi A katika mtihani wa taifa wa darasa la nne.

Hii inaendeleza mafanikio mazuri ya kitaalamu kwenye shule hiyo. Mwaka 2006 wanafunzi wote 20 wa darasa la nne na wanafunzi 70 kati ya wanafunzi 71 wa darasa la saba kwenye shule hiyo walishinda mitihani ya kitaifa.

Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Margaret Lewis, katika ripoti yake ya hivi karibuni, ameeleza kuwa darasa la nne la mwaka 2006 lilikuwa ndilo la kwanza kufanya mtihani wa taifa wa darasa la nne tangu shule hiyo ianze kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Awali, lugha ya kufundishia kwenye Shule ya Mwadui 'A' ilikuwa ni Kiswahili.

Shule hiyo inagharamiwa na kuendeshwa na WDL.

TANGAZO LA MAZINGIRA

SIKU YA KUPANDA MITI MWADUI MPYA

"Siku ya upandaji miti katika Mwadui Mpya" imepangwa kufanyika Jumamosi, tarehe 16 Februari 2008. Mwadui sio tu ni mahali tunapofanyia kazi bali pia ni sehemu tunapoishi. Lengo la siku hii ni kupanda kiasi cha miti elfu nne kwenye eneo la hifadhi (uwanja zamani wa golf), na kuonyesha kuwa tunaona fahari na mji wetu wa Mwadui.

Tunakaribisha wakazi wote wa Mwadui, wakiwemo wafanyakazi wa idara zote za WDL na wa makampuni ya wakandarasi, kushiriki katika siku hii ya kwanza ya kupanda miti.

Viburudisho vitatolewa kwa washiriki baada ya kumalizika kwa shughuli hiyo ya kupanda miti. Tunatarajia kushiriki kwako siku hiyo.

Tafadhari zingatia: Taarifa zaidi zitatolewa jinsi siku hiyo itavyokaribia, zikiwa ni pamoja na zinazohusu mahali pa washiriki kukutana, wakati gani, n.k.

Danie Smit
Meneja wa Mgodi

Kama unayo habari au picha inayostahili kuchapishwa kwenye Mwadui Mpya, wasiliana na Mhariri: Ray Ishengoma, Simu: 0755 076587. Baruapepe: ishengomaray@yahoo.com

Wajasiriamali wanawake, sehemu muhimu ya jamii ya Mwadui

Wakati mara nyingi huchukulia jitihada zao njia tu ya kuongeza pato la familia zao, wajasiriamali wadogo wanawake wanatoa huduma muhimu kwa jamii ya Mgodi wa Mwadui.

Kutokana na mazingira ya kipekee ya mji wa mgodi, ambako wengi wa wakazi wake ni wafanyakazi wa mgodi na makampuni yanayofanya kazi za kikandarasi, kwa kiasi kikubwa ni wanawake, ambao huendesha biashara kwenye maduka na vibanda katika maeneo yaliyotengwa na menejimenti ya mgodi kwa ajili ya shughuli hizo.

Akina mama hawa, wengi wao wakiwa ni wake za wafanyakazi, huuza mboga mboga, matunda, vyakula, nguo na vifaa vya nyumbani..

Katika mahojiano ya hivi karibuni, baadhi ya wanawake hao walisema kuwa waliamua kuanzisha biashara ili kuepuka kutegemea mapato ya waume zao pekee. Biashara hizi zinawawezesha kuchangia matunzo ya familia zao.

"Kama unavyofahamu gharama za chakula na elimu ya watoto zinazidi kupanda.. Umewadia wakati wanawake kutobaki wamebweteka. Biashara zetu zimesaidia sana katika kuboresha maisha ya familia zetu," alisema Mama Regina Richard. Ni mmoja wa akina mama wenye maduka kwenye eneo lijulikanalo kama Kompaundi, lililopo mashariki mwa mji wa Mwadui.

Mama Josephine Dadu, mmiliki mwingine wa duka kwenye eneo hilo, alidakia: "Licha ya kupunguza makali ya maisha, pato linalotokana na biashara zetu ndogo mara nyingi husaidia wakati dharura kama kifo cha ndugu zinapotokea. Wakati mwingine waume zetu huwa hawana fedha za kutosha kunapojiri tukio kama hilo, ambalo wakati mwingine hulazimu kusafiri mbali."

Hata hivyo, akina mama hao walidai kuwa wanakabiliwa na changamoto kadhaa katika kuendesha na kupanua biashara zao, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na mitaji ya kutosha, gharama kubwa za umeme na kuongezeka kwa wachuuzi, wajulikanao kama 'machinga', katika eneo la mji.

Walisema ili waweze kuongeza mitaji yao, huchukua mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha kama FINCA, Pride na mabenki. Hata hivyo, walilalamika kuwa riba zinazotozwa na taasisi hizi ni kubwa mno.

Ijapokuwa wanawake hao wanakiri kwamba kuanzisha chama chao cha kuweka na kukopa ndiyo njia bora ya kupanua biashara zao, wanasema kuwa hawajachukua hatua hiyo kwa sababu wengi wao hawana ujuzi wa kuanzisha chama kama hicho na hawafahamu kitakuwa na manufaa gani kwa wanachama.

Uongozi wa mgodi umekubali kuwaunganisha wajasiriamali wadogo kama hao na mashirika ambayo yanaweza kuwasaidia kuanzisha chama cha kuweka na kukopa na kuwapatia mafunzo. Hili ni mojawapo ya masuala yatakayojadiliwa kwenye Jukwaa la Jamii ya Mwadui Mpya litakalofanyika mwezi Machi, mwaka huu.

Mfuko wa Elimu wa Wafanyakazi wa WDL wakopesha Sh. Mil. 186

Mfuko wa elimu wa wafanyakazi wa WDL umetoa mikopo ya thamani ya zaidi ya shilingi milioni 186 tangu ulipoanzishwa mwaka 2005.

Katibu wa mfuko huo, Ramadhan Kilao, amesema mfuko huo ulianzishwa ili kuwasaidia wafanyakazi wa kampuni kumudu gharama za elimu ya watoto wao. Ameeleza kuwa kwa kuwa gharama hizi zinazidi kupanda wakati mwingine ni vigumu kwa wafanyakazi kutegemea mishahara yao pekee kuzimudu.

Kilao ameishukuru menejimenti ya WDL kwa msaada ilioutoa katika kuanzisha mfuko huu, ambao ni pamoja na kuupatia dola za Kimarekani 5,000 zikiwa ni mtaji wa kuanzia.

Hadi Aprili, 2008, mtaji wa mfuko utakuwa umefikia zaidi ya shilingi milioni 58. Wafanyakazi wote wa WDL wanaruhusiwa kujiunga na mfuko na hivi sasa unao wanachama 148.

Kuanzia mwezi Aprili, mwaka huu, ada ya uanachama itakuwa ni shilingi 350,000. Mfuko hutoa mikopo yenye thamani ya hadi mishahara ya miezi mitatu ya mwanachama. Mikopo hurejeshwa katika kipindi cha miezi 12 na riba yake ni asilimia tano.

Uzalishaji chini Desemba, Januari

Usafishaji wa mchanga wenye almasi kwenye vinu vyote vitatu katika miezi ya Desemba 2007 na Januari mwaka huu ulikuwa tani 105,435 chini ya lengo la tani 586,338. Tani za mchanga zilizosafishwa katika kipindi hicho ni 480,903.

Kiasi cha karati za almasi zilizopatikana zilikuwa chini ya malengo kwa asilimia 28.8 mwezi Desemba na asilimia 26.1 mwezi Januari.

Miongoni mwa sababu zilizokwamisha uzalishaji ni mchanga wenye matope, mvua kubwa na kuziba kwa sehemu za vinu.

Wafanyakazi wanne wastaafu kazi WDL

Wafanyakazi wanne wa WDL wamestaafu kazi kuanzia mwishoni mwa Desemba, mwaka jana, baada ya kutimiza umri wa kustaafu kwa lazima, wa miaka 60. Wote kwa pamoja wakiwa wameitumikia WDL kwa miaka 112.

Lucas Kasiga, aliyekuwa msimamizi wa karakana, ameitumikia kampuni kwa miaka 39.

Elisante Gerison, ambaye alikuwa opereta kwenye kinu cha kuzalisha umeme, amestaafu baada kuitumikia kampuni kwa miaka 37.

Kasiga Jilala, aliajiriwa kama dereva, akiwa amejiunga na kampuni mwaka 1990.

Jilala Kulwa, aliyekuwa akifanya kazi katika kinu cha kusafisha almasi, ameitumikia WDL kwa miaka 19.

Joseph Mhoja, mfanyakazi wa MPP na Felister Janga wa WDL wakiwa na nyuso za furaha walipofunga pingu za maisha hivi karibuni hapa Mwadui.

Wakazi wa Mwadui watahadharishwa kuhusu mbwa wanaozurura

Menejimenti ya WDL ina wasiwasi kuhusu ongezeko la mbwa wanaozurura mjini Mwadui, ambao baadhi yao waliachwa nyuma na wafanyakazi walioondoka na wakandarasi.

Uongozi wa WDL umeamuru kwamba wakazi wote wa mgodini kusajili mbwa wao. Mbwa watakaokutwa wakizurura mjini watapigwa risasi.

Zaidi ya hiyo, mbwa wote sasa wanatakiwa kupatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa kimeta. Hii itagharimu shilingi 1,500 kwa kila mbwa na tarehe ya kuanza kutolewa chanjo hiyo itatangazwa hivi karibuni na Idara ya Usalama, Afya na Mazingira